# Muziki wa Bongo Fleva na Changamoto za Kimaadili katika Jamii

*R. T. Kadallah*

**Ikisiri**

Makala haya yanajadili na kudadisi mojawapo ya changamoto za kimaadili zinazowakabili wapenzi na wadau mbalimbali wa muziki wa Bongo Fleva. Shabaha ya kuzuka kwa mjadala wa namna hii imeletwa na hali ya mabadiliko ya ukubalifu wa sanaa yenyewe kwa jamii. Kihistoria, sanaa hii ilihusishwa na makundi ya vijana, hususani vijana wasiokuwa na ajira. Tafiti za hivi karibuni kuhusu muziki wa Bongo Fleva zinaonesha kuwa wasanii na wadau wengine wa sanaa hii wanajivunia kukubalika kwa kiwango kikubwa zaidi, pengine kuliko aina nyinginezo za miziki. Tunaelezwa kuwa upokezi wa muziki huu kwa jamii umevuka mipaka ya kijinsia, kiarika na kitaifa kiasi kwamba leo hii Bongo Fleva ni sanaa inayopendwa sio tu na vijana bali pia na wazee, ambao hapo mwanzo hawakuikubali kabisa. Kukubalika kwa sanaa hii kunatokana na ujumi wa fani na maudhui ya sanaa husika. Hata hivyo, ndani ya kukubalika kwake, zimezuka changamoto anuwai za kimaadili. Katika makala haya changamoto husika zimejadiliwa sanjari na njia zinazotumika kusambazia muziki husika katika muktadha wa kiutandawazi na kidijitali.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yanahusu changamoto za kimaadili wanazokabiliana nazo wadau na wapenzi wa sanaa ya muziki wa Bongo Fleva. Kwamba, ingawa sanaa hii inakua na kukubalika kwa kasi zaidi katika nchi za Afrika Mashariki, yaani Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda bado sanaa hii haijafanyiwa tathmini ya kutosha kuhusu jinsi gani inaweza kukidhi matakwa ya wapenzi wake bila kuharibu mustakabali wa maadili ya wanajamii.

Katika kujadili mada hii, kwanza tumezungumzia juu ya sanaa ya muziki kwa ujumla kwa kuzingatia dhima yake katika jamii. Pili, tunaelezea etimolojia na maudhui ya muziki wa Bongo Fleva. Mwisho, tumefanya mjadala kuhusu changamoto za kimaadili zinazowakabili wadau wa sanaa ya muziki huu. Swali la msingi katika mjadala huu ni Je, ni kwa kiwango gani sanaa ya muziki wa Bongo Fleva inakidhi matakwa ya wanajamii kimaadili? Kama sivyo tufanyeje?

## 2.0 Dhima ya Muziki katika Jamii

Sanaa ya muziki ni muhimu kama zilivyo sanaa nyinginezo. Muziki husaidia katika masuala ya kijamii kama kuburudisha, kuunganisha, kutambulisha na kuelimisha jamii. Kwa ujumla, muziki husaidia katika suala la ujamiishaji wa wanajamii. Miongoni mwa maeneo ambayo sanaa ya muziki inatumika sana ni pamoja na dini, ibada za kimatambiko na sanaa za maonesho. Hivyo, muziki

una dhima kubwa katika jamii ikiwemo kuelimisha. Mathalani, katika nchi za Marekani ya Kaskazini na Ulaya, muziki unatumika katika kufundishia kutoka umri kabla ya shule hadi kiwango cha elimu baada ya sekondari. Hii ni kwa sababu muziki unahesabika kuwa na uwezo wa kutengeneza mazingira mazuri ya kujifunzia (Woodall na Ziembroski, 2002). Wakielezea kuhusu umuhimu wa sanaa ya muziki katika kuhamasisha na kuelimisha wanajamii Bergethon and Boardman (1963:18) wanasema:

> *There is no humans struggle for existence that has not been accompanied, communicated and completed by music.*
> [Hakuna harakati zozote za maisha ya binadamu ambazo haziambatani, kuwasilishwa au kukamilishwa na muziki (tafsiri yetu)].

Pia, kama ilivyofafanuliwa na Campbell (2004: 19) kuwa Martin L. King (1483-1546), ambaye ni mchungaji wa zamani na mwanaharakati katika mapinduzi ya kidini anaamini kuwa:

> *The moral, temperamental, intellectual and spiritual nature of the people improved through music.*
> [Maadili, hulka, akili na hali ya kiroho ya watu huboreshwa kupitia muziki (tafsiri yetu)].

Ni dhahiri kuwa kwa mifano hii michache muziki una dhima kubwa katika jamii. Jambo hili pia linajadiliwa na msanii nguli wa muziki wa dansi na baadaye injili hayati Remmy Ongala katika wimbo wake 'Muziki Asili yake Wapi?'

## 3.0 Muziki wa Bongo Fleva: Etimolojia na Maudhui yake

Kietimolojia, Bongo Fleva ni neno lililotokana na muunganiko wa maneno mawili ya lugha mbili tofauti, kuna neno la Kiswahili 'Bongo' na kuna neno la lugha ya Kingereza 'Flavor'. Bongo maana yake ni akili na Flavor, ambalo katika Kiswahili limetoholewa matamshi yake na kuwa Fleva, hufasiriwa kama ladha. Kwa hiyo, fasili ya kwanza ya muziki wa Bongo Fleva ni ladha zitokanazo na matumizi ya akili. Hata hivyo hii ni fasili finyu ya Bongo Fleva, fasili pana inayofaa ni ile ya kisitiari. Katika mtazamo huu, Bongo, hurejelea jiji la Dar es Salaam au Tanzania kwa ujumla. Istilahi hii ilizuka tu kama sehemu ya utashi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili, hasa kutokana na kuongezeka kwa hali ngumu katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, ambapo ili mtu aweze kujikimu anahitaji kutumia akili na maarifa mengi zaidi kuliko ambavyo angetumia akiwa pembezoni mwa miji hiyo mikubwa.

Nchini Tanzania muziki huu umetokea katika miaka ya 1980 (Mwanjoka, 2011). Kukua na kuzuka kwa muziki huu kumetokana na mitindo ya muziki wa aina mbalimbali kama vile muziki wa *Hip hop*, Rap, RnB, Zouk, Charanga, Rhumba, Raga, ngoma za asili na muziki wa Kikongo. Licha ya kuwa muziki huu una mchanganyiko wa mitindo ya muziki wa aina mbalimbali, jina kuu la muziki huu, nchini Tanzania ni muziki wa *Hip hop*, Bongo Fleva na Muziki wa Kizazi Kipya. Kimaudhui, muziki huu unazungukia takribani nyanja zote za kimaisha japo katika viwango na msisitizo tofautitofauti. Miongoni mwa dhamira zinazojadiliwa ndani ya muziki wa Bongo Fleva ni pamoja na siasa, uchumi, afya, na masuala ya uhusiano. Aidha, kutokana na umaarufu na maudhui yake, muziki huu sasa sio tu kwamba ni muziki wa vijana bali pia ni muziki wa kijamii kwani unawavutia hata wazee, ambao hapo mwanzo hawakuuthamini na waliuona kuwa ni muziki wa vijana, wa kihuni na haufai katika jamii (taz. pia Omari, 2009; Mwanjoka, 2011; Samwel, 2012).

**4.0 Changamoto za Kimaadili kutoka Muziki wa Bongo Fleva**

Kimsingi pamoja na faida nyingi za muziki wa Bongo Fleva, kuna changamoto mbalimbali zinazotokana na sanaa yenyewe ya muziki, njia za usambazaji wa sanaa hiyo na muktadha wake wa utendekaji. Kwa desturi, sanaa ya muziki wa Bongo Fleva inawahitaji wasanii wake wawe wabunifu vya kutosha ili katika kuelimisha kwake kuwepo na upya wa namna fulani. Hali hii huwaongezea wasanii wapenzi na kipato. Kwa ujumla hali hii ndio inayoufanya muziki huu upendwe na watu wengi. Mojawapo ya vipengele vya kisanii ambavyo vinafanyiwa ubunifu ni pamoja na mavazi, miondoko na unenguaji. Mathalan, vijana wengi wanavaa suruali kwa kuning'iniza makalioni badala ya kuvalia kiunoni kama ilivyo desturi. Mtindo huu wa uvaaji unaitwa 'Kata Kundu' au kwa kifupi wanasema 'Kata K'. Hali hii huwafanya wavaaji waonekane kama vile suruali zao zinaanguka, na pengine huanguka kweli.

Kwa upande wa wanamuziki wa kike, kuna tatizo zaidi kuliko wanamuziki wa kiume, hasa katika mavazi. Ingawa si wote, idadi kubwa ya wanamuziki wa kike wa Bongo Fleva mavazi yao yanaleta 'kinyaa' kwa sababu wanadhani kuwa kudhihirisha sehemu ya miili yao kama vile vitovu, mapaja, migongo na matumbo ndio jambo zuri. Ikiwa lengo la mavazi ni kusitiri maungo ya mwanadamu isipokuwa katika muktadha maalumu, basi wasanii hawa wanaigiza wakiwa nusu uchi. Kwa ufupi, wasanii hawa haielekei kuwa wamevaa au hawajavaa. Swali ni je, jamii ijifunze kitu gani kutokana na uvaaji wao?

Vijana na watoto ambao ndio wapenzi wakubwa wa muziki huu nao huiga tabia hizi, na mwisho tunaona kuongezeka kwa vitendo vya kifuska. Suala hili pia

linahusiana sana na masuala ya elimu ya afya dhidi ya UKIMWI. Sambamba na suala hili, wasanii wa Bongo Fleva pia wanajibainisha kwa kuwa na ubunifu wa miondoko ya namna tofautitofauti. Ilimradi kuwepo na ustadi utakaosaidia kuleta burudani na kuwa kivutio kwa mashabiki wa sanaa husika. Mojawapo ya mitindo ya miondoko hiyo ni kutembea kwa hali ya kuruka ruka au kudundika, hali inayoashiria kujiamini kwa hali ya juu. Hata hivyo kujiamini si jambo baya.

Changamoto nyingine ya muziki huu inajitokeza katika suala la unenguaji. Unenguaji ni suala muhimu katika muziki wa Bongo Fleva. Wasanii huchezesha na kuviringisha sehemu za miili yao kama vile vichwa, mikono, miguu na viuno (taz. Masonga, 2005; Omari, 2009 na Samwel, 2012). Ni kweli kuwa sanaa ya unenguaji husaidia kuboresha afya na kuifanya miili ya wasanii isishambuliwe na maradhi kiurahisi. Hata hivyo, kitendo cha kuipamba sanaa hii kwa unenguaji kina dosari kadhaa. Mosi, kwa kiwango kikubwa wasanii, hasa wa kike, wananengua sehemu ya kiunoni; suala hili linaleta hisia za starehe za ngono. Kutokana na hili, sanaa ya muziki wa Bongo Fleva, inaonekana kuwa ni sanaa ya wahuni na sanaa ya watu wasiojali maadili ya wanajamii. Aidha, kuna lawama kuwa hata kasi ya kuongezeka kwa maambukizi ya maradhi ya UKIMWI inatokana na kusisitiza unenguaji huo unaofanywa katika majukwaa bila kificho chochote.

Madai kuwa Bongo Fleva ni muziki wa wahuni linashadidiwa na namna maudhui yake yanavyoegemea kwenye suala la mapenzi zaidi kuliko dhamira nyinginezo. Takribani kila msanii hujiona kuwa bado hajafanya chochote kama hajatengeneza wimbo unaohusu mapenzi. Pia, lugha inayotumika katika muziki huu inaonekana kuleta utata na changamoto za kimaadili. Sehemu kubwa ya msamiati wa lugha ya muziki wa Bongo Fleva imejaa lugha ya mitaani, maneno ya kebehi na matusi. Ingawa muziki huu unasaidia katika kuhifadhi lugha ya wanajamii lakini ipo haja kwa wasanii kufikiria namna bora ya uwasilishaji na uhifadhi wa lugha ya wanajamii. Kizazi kilichopo na hata kizazi kijacho, kinahitaji muongozo sahihi wa namna ya kujifunza lugha yao.

## 5.0 Changamoto za Usambazaji wa Muziki wa Bongo Fleva

Miongoni mwa njia zitumikazo na muziki huu kuwafikia wanajamii ni vyombo vya habari kama vile redio, magazeti, televisheni na mitandao. Njia zote hizi zinachangia sana katika kuufanya muziki huu ufahamike na kupata umaarufu sio tu katika miji mikubwa bali, pia hata katika miji midogo na vijiji. Si jambo baya kukiwa na nyenzo sahihi za kuwawezesha wasanii kuwasiliana na wanajamii kwa haraka na ufanisi zaidi. Hata hivyo, njia hizi husababisha muziki wa Bongo Fleva uwe na dosari mbalimbali kama ifuatavyo:

Kutokana na ukweli kuwa vyombo vya habari vinaendeshwa kibiashara hata namna ya uwasilishaji wa sanaa husika huelekea kuwa wa kibiashara zaidi. Kwa hali hiyo basi, kuna ukasuku mwingi unaozitangaza na kuzisambaza nyimbo za wasanii wa Bongo Fleva. Hakuna nafasi ya kuweka wazi ubora na upungufu wa muziki fulani. Kuna muelekeo kuwa, nyimbo zote za muziki wa Bongo Fleva ni nzuri na bora na hazina upungufu wowote. Kimsingi, kila kitu kizuri kina dosari zake, haiyumkini kuwa sahihi kutotaja wala kutojadili dosari za muziki wa Bongo Fleva.

Changamoto nyingine katika suala hili ni kuwa kutokana na ukweli kuwa vyombo vinavyotumika vinatuweka katika hali ya maisha ya kiutandawazi, inakuwa vigumu kufanya ubainishaji ulio sahihi katika kufundisha na kutoa maadili katika jamii. Kwa mfano, dhamira na masuala ambayo yalipaswa kutolewa kwa watu wazima badala yake yanatolewa katika hali ambayo haiwezekani kuitenganisha hadhira. Watoto na watu wazima wote wanafundishwa masuala yanayofanana, tena kwa njia moja. Suala la mapenzi, familia, talaka na masuala mengine kama haya ni mifano mizuri ya dhamira ambazo zilihitaji kutenganishwa miongoni mwa wanajamii. Suala lolote la kiujamiishaji linatazamiwa kuwa na mafanikio endapo litazingatia muda. Kwa hiyo, si sahihi kwa watoto wa umri mdogo kuhusishwa na mijadala ya masuala mazito na nyeti, badala yake kila kundi linahitaji elimu mahususi katika muda mahususi. Kutokana na changamoto kama hizi, watoto wanashindwa kumaizi nafasi na wajibu wao katika masuala wanayohubiriwa kila siku kupitia vyombo hivyo. Hatimaye, kuna mfumuko mkubwa wa mmomonyoko wa kimaadili miongoni mwa jamii za vijana. Mmomonyoko huo unajidhihirisha katika masuala kama vile, kuongezeka kwa vitendo viovu vya matumizi ya madawa ya kulevya, uasherati, ujambazi na masuala kadha wa kadha.

Changamoto hii ni kubwa kiasi kwamba kuna suala la uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kusambaa kwa vigenge vya burudani kila eneo na kila wakati. Kwa mfano, katika miji mikubwa kama Dar es Salaam kuna kelele zisizo kifani zinayosikika nyakati za usiku na hata mchana. Sababu ya tatizo hili ni kuwa, wanamuziki na wapenzi wengine wa muziki wa Bongo Fleva hawajali mahitaji na shida za watu wengine. Kwao, kila wakati na kila mtu anahitaji kuburudishwa kwa kupigiwa kelele za ngoma na sauti za Kibongo Fleva. Kiustaarabu kuna maeneo maalumu yaliyotengwa na yanayofahamika kuwa ni mahususi kwa ajili ya burudani na starehe za kila namna. Hata hivyo, hali halisi ni kwamba wanamuziki huenda popote pale watakapoalikwa ili mradi wahakikishiwe kuwa watalipwa.

Aidha, kutokana na kuwepo na uhuru kwa kila mtu kuwa na chombo chake kama vile radio au televisheni kuanzia miaka ya 1990, basi kila mtu ananunua kanda za muziki anazozipenda na kusikiliza mahali atakapo kwa wakati autakao. Kwa ufupi, muziki wa Bongo Fleva, unakabiliwa na changamoto ya kutokuwapo kwa mipaka ya utendaji na umiliki wa kazi zinazotokana na akili za wasanii.

**6.0 Hitimisho**

Katika makala haya tumedokeza nafasi ya muziki wa Bongo Fleva katika kuimarisha maadili ya jamii husika. Tumesisitiza kuwa ili kuifanya sanaa hii iwe nyenzo muafaka ya kimaadili hapana budi kufanywa uchunguzi yakinifu. Ingawa uchunguzi wa namna hii unaweza kuwa na mawanda mapana mno kiasi cha kuwakatisha tamaa wadau wake, lakini ni dhahiri kuwa haja ya kufanya hivyo ipo, na kila mdau bila kujali tasnia yake ana nafasi adhimu ya kuendeleza uchunguzi huu.

## Marejeleo


Anderson, William M. and Patricia Shehan Campbell, (eds), (1989), *Multicultural Perspectivesin Music Education*. Reston, VA: Music Educators National Conference.

Campbell, Patricia Shehan, (2004), *Teaching Music Globally*. New York: Oxford University Press.

Masonga, M. (2005), The Dramatic Elements in Bong Fleva Musical Video Production: A case study of Starehe (Ferooz) Nitakufaje (Crazy G.K) and Siamini (TID) unpublished MA Dissertation, University of Dar es Salaam.

Mwanjoka, Gerald. (2011). *Harakati za Bongo Fleva na Mapinduzi*. Dar es Salaam: Hakuna Mchapaji.

Omari, S. (2006), "Mitindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya" katika *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Juz. 69, kur. 73-92.

Omari, S. (2009). Tanzanian Hip hop poetry as popular literature. Ph.D Thesis (Literature) University of Dar es Salaam

Samwel, M. (2012). "Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva." (Haijachapishwa), Tasinifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Woodall, Laura and Brenda Ziembroski, (2002). Promoting Literacy Through Music, katika http://www.songsforteaching.com/lb/literacymusic.htm iliyosomwa tarehe 20/05/2010.